## MAENDELEO YA SEKTA YA MISITU NA NYUKI KATIKA MKOA

Mkoa una misitu ya asili inayokadiriwa kuwa na Hekta **239,454.54** na misitu ya kupandwa Hekta **369,400** na kufanya jumla ya Hekta **608,854.54** sawa na asilimia **28.75** ya ardhi yote katika mkoa wa Njombe.

Sekta hii imeendelea kukua mwaka hadi mwaka kutokana na hali ya hewa nzuri kwa ajili ya kilimo cha miti na mwamko mkubwa wa wananchi katika kulima miti kama zao la biashara kwa ajili ya matumizi mbalimbali mfano mbao, kuni, nguzo, mkaa, magome ya miti n.k .Kilimo cha miti inayolimwa au kupandwa zaidi kwa Mkoa huu ni ya aina tatu ambayo ni misindano (Pines spp) kwa ajili ya uzalisha wa mbao laini (Soft woods), milingoti (Eucalyptus spp) kwa ajili ya uzalishajiwa mbao ngumu (Hard woods) na nguzo na miwati (Black wattle – *Acacia meansii*) kwa ajili ya uzalishaji wa madawa ya ngozi, nguzo, kuni, mkaa n.k

## UMILIKI WA MISITU

Umiliki wa misitu kwa Mkoa huu, umegawanyika katika katika makundi tofauti kulingana na aina ya msitu. Misitu ya kupandwa inamilikiwa na watu binafsi (kwa kiasi kikubwa), taasisi, vikundi na kampuni kama TANWAT yenye mashamba makubwa.

Misitu ya asili ni ile ya Hifadhi Taifa inayomilikiwa na Wakala wa huduma za Misitu (TFS – Tanzania Forest Service Agency), Halmashauri za Wilaya, Vijiji na watu binafsi pamoja na misitu iliyopo katika Safu za Milima ya Livingstone na Kipengere. Misitu iliyo mingi ya asili imetambuliwa lakini haijapimwa ukubwa wake halisi, hii ni kutokana na ufinyu wa rasilimali (fedha na wataalam).

## HALI YA UPANDAJI MITI

Kampeni ya upandaji miti imeendelea kutekelezwa kila mwaka mkoani ambapo upandaji wa miti huanza mwezi Disemba mwishoni hadi kufikia mwezi Februari mwishoni katika maeneo mbalimbali. Aidha, halmashauri zote za mkoa wa Njombe zimekuwa zikivuka lengo lililotolewa na Serikali la kizitaka kila Halmashauri nchini kupanda miti isiyopungua 1,500,000 kila mwaka. Wastani wa zaidi ya miche ya miti 40,000,000 hupandwa kila mwaka katika Halmashauri za Mkoa huu.

Hali ya utunzaji wa miti iliyopandwa kwa ujumla ni nzuri licha ya changomoto hasa uchomaji moto ovyo wa mapori na misitu, ukame kwa baadhi ya maeneo n.k.

Kwa mwaka 2018 jumla ya miche 34,146,325 ilipandwa mkoani, kati ya hiyo 28,412,405 imepona sawa na asilimia 83 ya miti iliyopandwa. Kila mwaka uzinduzi wa upandaji miti Kimkoa na Kiwilaya hufanyika kama sehemu ya kampeni ya uhamasishaji kwa wananchi. Uzinduzi huu hufanywa na viongozi wa Mkoa na Wilaya katika maeneo yao.

(**Picha ya shamba bora la Miti**)

## USHIRIKISHWAJI WA JAMII KATIKA KUHIFADHI MISITU YA ASILI

Katika kuhifadhi misitu ya asili na Bioanoai (Biodiversty), ushirikishwaji wa wananchi hutumika kama njia muhimu sana ya uhifadhi. Serikali kupitia program mbalimbali kama vile Usimamizi Shirikishi wa Misitu (Participatory Forest Management), wadau na mashirika mbalimbali imekuwa ikitumia dhana hii ya ushirikishwa wa wananchi katika masuala yanayohusu uhifadhi wa misitu kwa watu binafsi, vikundi, NGOs, serikali za vijiji na halmashauri.

Katika kushirikisha juu kuhifadhi misitu, jumla ya hekta **171,263.3** katia ya hekta **239,454.54** za misitu ya asili zimetengwa na kuhifadhiwa na serikali za vijiji vilivyopo ndani ya Mkoa kupitia program ya usimamizi shirikishi wa misitu (USM) na wadau wengine. Hata hivyo, elimu ya hifadhi ya mazingira imeendelea kutolewa kwa jamii ambapo Jumla ya vijiji **295** kati ya **381** katika mkoa vimewezeshwa kuandaa sheria ndogo za vijiji zinazohusu utunzaji wa maliasili na mazingira kupitia kamati za mazingira za vijiji husika. Aidha, Mkoa una wadau mbalimbali (Vikundi, NGos, CBOs, Taasisi n.k) wapatao **63** wanaojishughulisha na masula ya upandaji na uhifadhi wa misitu na mazingira.

## MCHANGO WA SEKTA YA MISITU KATIKA PATO LA MKOA

Misitu ina mchango mkubwa katika uchumi wa Mkoa ikiongozwa na zao la mahindi. Biashara ya mazao ya misitu imekuwa ikichangia sana pato la kaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla. Mfano mwaka 2015 wastani waasilimia 46 ya pato la mkoa ilichangiwa na sekta ya misitu.
Kwa mwaka 2017, zaidi ya shilingi bilioni 646.6 zilipatikana kutokana na biashara mbalimbali za mazao ya misitu hususani mbao, mkaa, magome/ magamba ya miti hasa kutoka kwenye misitu ya kupanda ya wananchi, taasisi na makampuni. Kutokana na biashara hiyo ya mazao ya misitu, Serikali Kuu imekuwa ukiingiza fedha nyingi kutokana na kukata leseni za biashara, tozo ya faini na kutoa vibali vya kusafirisha mazao ya misitu. Aidha, Halmashauri zimekuwa zikiongeza makusanyo ya mapato yatokanayo na asilimia tano (5%) kutokana na mazao ya misitu na hivyo kuifanya sekta hii kuwa chanzo muhimu cha mapato kwa serikali kuu na Halmashauri katika Mkoa.

Takwimu za NBS zinaonesha kuwa mchango wa sekta ya Misitu kwa Pato la Taifa mwaka 2017 ilikuwa ni shilingi trillion 4.7 sawa na asilimia 4 ya pato la Taifa.

## FURSA ZA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MISITU KATIKA MKOA WA NJOMBE

Mkoa una fursa nyingi za uwekezaji katika sekta ya misitu hususan katika viwanda vya uchakataji na uongezaji wa dhamani wa mazao ya misitu. Kutokana na uwepo mkubwa wa malighafi za misitu, miundombinu mizuri (barabara na mawasiliano), maeneo ya kutosha ya uwekezaji, umeme wa uhakika na nguvu kazi ya uhakika (Labourers) katika Wilaya zote za Mkoa, zipo fursa za kuwekeza katika viwanda vya utengenezaji wa samani mbalimbali (Furnitures, Plywoods, veneer etc), nguzo za kwa matumizi mbalimbali.Uwekezaji katika uzalishaji wa mkaa utokanao na mabaki mbalimbali yatokanayo na shughuli za uzaliashaji wa mazao ya miti mfano, vumbi la mbao (saw dusts) unaweza kufanyika pia.

## SEKTA YA UFUGAJI NYUKI

Mkoa una fursa nyingi za kuweza kuwekeza katika shughuli za ufugaji nyuki zikiwemo:-

1. Uwepo wa maeneo makubwa yaliyo na misitu ya asili na kupandwa inayoruhusu shughuli za ufugaji nyuki hali itakayowezesha kupata asali na mazao ya nyuki kutoka katika uoto mbalimbali mfano miombo, misitu ya lindimaji, miti ya matunda kama parachichi, matofaa, topito, fyulisi nk.
2. Uwepo wa mashamba ya mazao mbalimbali ya kilimo yanayoruhusu shughuli za ufugaji nyuki kama vile alizeti,viazi, maboga, mbogamboga nk.
3. Uwepo wa hali ya hewa inayoruhusu shughuli za ufugaji nyuki.
4. Uwepo wa miundombinu (barabara nyingi ambazo zinapitika misimu yote kutoka wilayani hadi mkoani)
5. Uwepo wa nishati ya umeme katika kila Makao Makuu ya Wilaya na idadi kubwa ya vijiji kupitia program ya REA III.
6. Uwepo wa wataalamu ngazi ya Halmashuri na Mkoa
7. Uwepo wa sera, sheria na kanuni zinazoruhusu shughuli za ufugaji nyuki katika Mkoa.
8. Uwepo wa Wataalamu wa kutengeneza zana za kuendeshea shughuli za ufugaji nyuki kama vile mizinga na mavazi ya kujikinga.
9. Uwepo wa makundi mengi ya nyuki sehemu mbalimbali katika Mkoa.

**Mwitiko wa Wananchi katika Kutekeza Shughuli za Ufugaji wa Nyuki.**
Mwitiko wa wananchi katika kutekeleza shughuli za ufugaji wa nyuki ni mkubwa japokuwa changamoto ni nyingi. Hadi kufikia mwaka 2018/2019 Mkoa una jumla ya mizinga **22,022** ya kienyeji na **17,048** ya kisasa, ambapo jumla ya lita **104,854** za asali na kilo **4,392** za nta zilizalishwa. Jedwali namba 4 hapo chini linaonesha kwa kina idadi ya mizinga, idadi ya vikundi vya wafugaji nyuki, kiasi cha asali kilichozalishwa na kilo za nta kwa kila Halmashauri.

**Jedwali Na: 1 Uzalishaji wa Asali Mkoa wa Njombe kwa Mwaka 2018/2019**

| **Halmashauri** | **Idadi ya Mizinga** | | **Idadi ya Vikundi vya Ufugaji Nyuki** | **Uzalishaji wa zao la Asali na Nta 2018/19** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Kienyeji** | **Kisasa** | | **Asali (Lita)** | **Nta(Kg)** |
| Njombe DC | 4,817 | 3,271 | 29 | 27,200 | 1,200 |
| Njombe TC | 643 | 1,481 | 22 | 6,122 | 413 |
| Ludewa DC | 11,600 | 5,292 | 27 | 40,971 | 1,986 |
| Makete DC | 384 | 3,672 | 18 | 13,879 | 205 |
| Makambako TC | 150 | 186 | 2 | 180 | 70 |
| Wanging'ombe DC | 4,428 | 3,146 | 36 | 16,502.00 | 518 |
| **JUMLA** | **22,022** | **17,048** | **134** | **104,854** | **4,392** |

*Chanzo: Halmashauri za Mkoa wa Njombe, 2019*

**Mkakati wa Mkoa wa Njombe Katika Ukuzaji wa Shughuli za Ufugaji Nyuki**

Mkoa wa Njombe una mkakati wa kukuza shughuli za ufugaji nyuki kama ifuatavyo:-

1. Kuendelea kutoa elimu na hamasa juu ya umuhimu wa shughuli za ufugaji nyuki kiuchumi katika wilaya zote nne za Makete, Njombe, Wanging’ombe na Ludewa.
2. Kuwaunganisha wadau mbalimbali wa shughuli za ufugaji nyuki ili kukuza sekta ya ufugaji nyuki.
3. Kutafuta wahisani/ wawekezaji katika shughuli za ufugaji nyuki.
4. Kuwatambua wafugaji na kuwaunganisha katika vikundi ili wapate elimu kiurahisi na waweze kutafuta masoko na kupanga bei ya mazao ya nyuki.
5. Kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za ugani kwa watumishi wa kada mbalimbali mkoani ili kukuza uelewa katika utekelezaji wa shughuli za ufugaji nyuki.
6. Kuandaa mpango wa kuwajengea uwezo watumishi mbalimbali waliopo hadi ngazi ya Kijiji ili waweze kusaidia katika utekelezaji wa shughuli za ufugaji nyuki.
7. Kuandaa vipeperushi vinavyoeleza umuhimu wa matumizi ya mazao ya nyuki na kuvisambaza ili kukuza soko la mazao hayo.
8. Kutoa elimu na kutafuta masoko ya mazao na huduma za nyuki ambazo hazitumiki kwa kiwango cha kutosha mfano huduma za uchavushaji na mazao kama nta, chavua, sumu ya nyuki na gundi ya nyuki.
9. Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wa ufugaji nyuki ili kuweza kupata mahitaji ya bidhaa za ufugaji wa nyuki Mkoani mfano Mafundi seremala kwa ajili ya utengenezaji wa mizinga, mafundi kushona kwa ajili ya ushonaji wa mavazi ya kujikinga na mafundi uashi kwa ajili ya kutengeneza mabomba ya moshi pamoja na patasi za mizinga.
10. Kuwaunganisha wafugaji wa nyuki na taasisi zinazotengeneza vifungashio.
11. Kuhakikisha mazao ya nyuki yanafika sokoni yakiwa na ubora unaotakiwa kwa kuhamasisha uanzishwaji wa wajasiriamali kuanzisha Viwanda vya kufungashia asali.
12. Kuwaunganisha wafugaji na Taasisi zinazotoa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za ufugaji nyuki